



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO



Unapojibu tafadhali taja

Kumb Na.: HWB/ F.10/176/165

Tarehe: 22 Oktoba, 2024

Watumishi Wote,  
Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo,  
S.L.P 59,  
**BAGAMOYO.**

**TANGAZO LA MKOPO KWA WATUMISHI WA UMMA HALMASHAURI YA WILAYA YA  
BAGAMOYO KWA MWEZI OKTOBA, 2024 TSHS. 350,000,000/=**

Kichwa cha habari chahusika.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imepokea Fedha Jumla ya Tshs. **350,000,000/=** kutoka Wizara ya Fedha ikiwa ni mwendelezo wa Mikopo inayoletwa kwa Watumishi wa Umma, kwa kuzingatia Waraka wenye **Kumb. Na. C/AC.7/228701/16** wa tarehe **30 Juni, 2021** kuhusu utaratibu wa kukopesha Fedha Taslimu Watumishi wa Serikali kwa ajili ya kununulia Magari, Pikipiki, Samani na Matengenezo ya Magari, na Pikipiki. Aidha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo Fedha hizi ni za awamu ya Tano (5).
3. Kwa Tangazo hili, mnajulishwa kwamba mnatakiwa kuwasilisha maombi yenu ya mkopo husika katika Mfumo wa mikopo ya Hazina unaoitwa "**Hazina Portal**" kupitia kujisajili kwenye Link "**als.muse.go.tz**" ili uweze kutengeneza akaunti na kuapply mkopo wako. Si zaidi ya tarehe **04 Novemba, 2024** saa **9.30** Alasiri. Kwa msaada wa usajili wasiliana na Mtaalam:-  
**Nawile Maokola – Afisa Utumishi Mkuu Simu Namba. 0713 42 36 99**
4. Aidha taarifa utakazingiza wakati utakapojisajili katika link tajwa hapo juu ziwe sawa sawa na taarifa zako zilizopo katika mfumo wa taarifa za Mishahara yaani e watumishi uliokuwa unajulikana kama "**NEW HCMIS**"

PKAM/UTUMISHI

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.  
Simu Na: +255 733860575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz). Tovuti: [www.bagamoyodc.go.tz](http://www.bagamoyodc.go.tz)

5. Masharti na vigezo vya Mkopo vinavyohitajika ni kama ifuatavyo:
- Lazima awe Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.
  - Mshahara wake usipungue  $\frac{1}{3}$  "Basic Salary"
  - Awe tayari kujaza Mkataba utakaotoka kwenye mfumo wa "Hazina Portal"
  - Kiwango cha Mkopo kitakachotolewa ni kile kitakachokuwa kimeidhinishwa na Kamati ya Mikopo itakayokuwa imeundwa na Mkurugenzi Mtendaji.
  - Asiwe mnufaika wa mkopo iliyotolewa ya Miaka 2020, 2021, 2022 na 2023
  - Maombi ya Mikopo yazingatie aina ya mkopo na viwango vilivyoainishwa katika jedwali.
6. Jedwali lenye mchanganuo wa mkopo limeambatanishwa.
7. Nawatakia utekelezaji mwema.

Shauri Selenda  
**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO**

NB:- Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Bagamoyo ambayo ni [www.bagamoyodc.go.tz](http://www.bagamoyodc.go.tz)



Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,  
Jitokeze Kushiriki Uchaguzi

VIWANGO VIPYA VYA MIKOPO YA FEDHA TASLIM.

NA	AINA YA MIKOPO	NGAZI YA MSHAHARA	KIWANGO CHA JUU CHA MIKOPO KINACHOPENDEKEZWA (TSHS)	MUDA WA MAREJESHO
1.	Mkopo wa fedha taslimu kwa ajili ya ununuzi wa magari, pikipiki, samani na matengenezo ya vyombo vya usafiri	TGS A-C, TGTS A-C, TGHS A-C, AGCS 1-2, TGHS A-C, SAIS A-C.	15,000,000/=	Miezi 72
		TGS D-F, TGTS D-F, TGHS D-F, AGCS 3-4, TJS 3-5, TGRS A-C, SAIS D-F	30,000,000/=	Miezi 72
		TGS G-H, TGTS G-H, TGHS G-H, AGCS 5-6, TJS 6, TGRS D-E, SAIS G-H	40,000,000/=	Miezi 72
		LSSE 1-4, TGTS I, TGHS I-J, AGCS 7-9, TJS 7-9, TGRS F-I, SAIS I-K	50,000,000/=	Miezi 72
		LSSE 5-9, TGHS K-L, AGCS 10-12, TJS 10-12, SAIS L-Q	55,000,000/=	Miezi 72